



MSAADAA KWA WATU WAZIMA

SIKU YA KIMATAIFA YA MAOMBI
KWA AJILI YA WAATHIRIKA WA
USA FIRISHAJI WA BINADAMU



KIINI CHA MAANDIKO

'Mwizi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.'
(Yohana 10:10).



KWANINI TUNA JUMAPILI HII MAALUMU?

Utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa Binadamu (UKUHB) ni nini? Jeshi la Wokovu limejitoa kikamilifu ili kukabiliana na utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu. Tuna mamlaka ya kitheolojia na kihistoria. Tunaamini maombi ni njia ya msingi na ya kipekee ya Jeshi la Wokovu kuitikia ili kuipata dunia iliyo huru na isiyokuwa na unyonyaji. Utumwa wa kileo hujitokeza kwasababu za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisheria ambazo hujenga mazingira magumu na hatarishi kwa wale wanaojikuta wamo katika utumwa. Hivi leo, kuna zaidi ya wanaume, wanawake na watoto milioni 40 duniani kote waliokumbwa na utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu. Kati ya hawa, zaidi ya milioni 15 wamo katika ndoa za kulazimishiwa, zaidi ya milioni 24 wamo katika kazi za kulazimishiwa na karibu asilimia 30 ya wanaonyonywa ni watoto.



JESHI LA WOKOVU LINAITIKIAJE SWALA HILI DUNIANI?

Tunaitikia kwa vitendo utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu katika nchi 108 kupitia kwenye maeneo yetu manane ya kukabiliana kivitendo: Maombi, Kuzuia, Kushiriki, Kulinda, Kushitaki, Ushirikiano, Sera na Ushahidi. Kila teritori/nchi ina mtu mhusika na ukuaji wa kazi katika maeneo haya nasi twakukaribisha kuungana na mwitikio huu. Mwaka 2021, tuliwahudumia na tukasafiri pamoja na walionusurika 9,795.



MDA WA MAOMBI YANAYOTAMKWA: Tafadhali tizama kwenye Msaada wa Maombi yanayotamkwa.



MAWAZO YA WIMBO (YAKIWA NA MISTARI YA MSINGI)

- (Katika Neema ya Yesu) 'Amazing Grace (Minyororo imeondolewa)
- ('Nimewekwa huru. Mungu wangu, mwokozi wangu amenifungua)
- 'Here I am to Worship' (Light of the world you stepped down into darkness)
- 'Light in the Darkness' (Be a light in the darkness, be a heart to the heartless)
- 'Way Maker' (Light in the darkness, my God that is who you are)
- 'In Christ Alone' (There in the ground his body lay, Light of the world by darkness slain, then bursting forth in glorious day, up from the grave he rose again)
- (Katika Neema ya Yesu) 'Amazing Grace' (Nilipotea dhambini, sasa nimepatikana, nilikuwa kipofu, sasa naona)
- 'There are People Hurting in the World out There' (They need you, they need me, they need Christ)
- 'I am No Longer a Slave to Fear' (We've been liberated from our bondage)



KUHUSU UJUMBE WA MAANDIKO NA KUTAFAKARI: Tafadhali tizama eneo la msaada wa Watu wazima, Vijana na Watoto.



MSAADAA KWA WATU WAZIMA

SIKU YA KIMATAIFA YA MAOMBI
KWA AJILI YA WAATHIRIKA WA
USA FIRISHAJI WA BINADAMU



MAOMBI YA UMOJA WA KUJITOlea:

Waalike waumini wako na wana jamii wajitoe ili wawe washirika katika mshikamano na wanusurika wa utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu.

Nasikia kilio cha mabinti na vijana wa kiume ng'ambo ya giza, waliosafirishwa na kufungwa utumwani kwa manufaa ya wengine.

Nasimama pamoja na wewe.

Naona kizazi kijacho cha watoto walio katika mazingira hatarishi wanaolengwa kwa ajili ya manufaa ya raha za ulimwengu.

Nitapigana kwa ajili yako.

Nasimama pamoja na wale walio mstari wa mbele, wakitetea waathirika wa ukandamizaji huu wapewe uhuru wao na wanaotembea pamoja na wanusurika.

Ninawatambua.

Naomboleza kwa ajili ya yale niliyochangia kwenye utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu kwa kuja au kutokujua kutokana na ujinga wangu, nafasi yangu na uwezo wangu wa matumizi.

Nakataa kuwa kipofu.

Naomba maombi yangu na yale ya watu wako yageuke kuwa tendo tunavyoendelea na mapambano dhidi ya maonevu pamoja.

Hatuko huru mpaka sote tuuone mwangaza.

Imeandikwa na Jean Nangwala, Zambia



CHAKULA CHA MCHANa

Mle chakula pamoja kisha mwendelee kutafakari juu ya upendo wa Mungu kwa wale ambaa ni waathirika wa utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu.



MAOMBI KWA VITENDO

Hapa pana mifano kadhaa ya jinsi wewe na kikao chako mnavyoweza kushiriki katika kuiheshimu siku hii zaidi ya ibada ya kawaida ya Jumapili:

- Panga pawepo maombi ya kutembea katika jamii yako.
- Waalike wana jamii yako waje kwenye Uchambuaji au Kujifunza Biblia/kiwe ni kikundi kidogo.
 - » Unaweza kufanya haya kivitendo kama hakuna vipingamizi au katika vikundi vidogo. Unaweza kufanya hivi kwa njia ya Mtandao wa WhatsApp, Zoom, Facebook au njia nyingine mtandaoni.
 - » Kumbuka kwamba unaweza kuchukua mafunzo toka kwingine mradi yaendane na jamii yako! Tafadhali tufikie kama unahitaji msaada juu ya haya.
- Endesha shughuli ya kufahamisha wengine kuhusu vyanzo au visababishi vyta ya usafirishaji haramu wa binadamu katika jamii yako. Wakaribishe wahusika wa idara hii toka katika teritori/kitaifa ili wawashirikishe kinachotakiwa ili wewe na kikao chako muweze kushiriki kikamilifu.